Kristo Hakunituma Kubatiza

(Christ Did Not Send Me To Baptize)

Na

Ellis P. Forsman

Kristo Hakunituma Kubatiza

(Christ Did Not Send Me To Baptize)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Kristo Hakunituma Kubatiza

1 Kor. 1:14-17

Pingamizi liliibuliwa kuhusu umuhimu wa ubatizo unaondana na kauli ya Paulo kwa kanisa la Korintho.

1 Kor. 1:14-17, "*Nashukuru kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu. Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana; zaidi ya hao sijui kama nalimbatiza mtu ye yote mwingine. Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri habari njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika.*"

Angalia maneno ya Paulo: 1 Kor. 1:17, "*Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri habari njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika.*" Ambayo wengine wanahitimisha kwamba ubatizo si lazima kwa wokovu.

Hataivyo, wakati mtu anapochukulia mazingira…

Mazingira ya ghafla ya maneno yake katika waraka.

1 Kor. 1:10-13, "*Basi ndugu nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana ndugu nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni wa Paulo, na mimi ni wa Apolo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni wa Kristo. Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au Je mlibatizwa kwa jina la Paulo?*"

Muktadha mbali ya huduma ya Paulo katika Korintho.

Mdo. 18:1-18, "*Baada ya mambo hayo Paulo akatoka Athene akafika Korintho. Akamwona Myahudi mmoja jina lake Akila, mzaliwa wa Ponto; naye amekuja kutoka nchi ya Italia siku za karibu pamoja na Prisila mkewe, kwa sababu Klaudio amewaamuru Wayahudi wote watoke Rumi, naye akafikilia kwao; na kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja, akakaa kwao wakafanya kazi pamoja, kwa maana walikuwa mafundi wa kushona hema. Akatoa hoja zake katika sinagogi kila ssabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani. Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo. Walipopingamana naye na*

kumtukana Mungu, akakung'uta mavazi yake akawaambia, damu yenu naa iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa. Akatoka huko akaingia katika nyumba ya mtu mmoja jina lake Tito Yusto, mcha Mungu, ambaye nyumba yake ilikuwa mpaka mmoja na sinagogi. Na Krispo mkuu wa sinagogi akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia, waliamini wakabatizwa. Bwana akamwambia Paulo kwa maono usiku, usiogope bali nena, wala usinyamaze, kwa kuwa mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakeyekushambulia ili kukudhuru; kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu. Akaa huko muda wa mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu. Hata Galio alipokuwa liwali wa Akaya, Wayahudi wakamwinukia Paulo kwa nia moja, wakamleta mbele ya kiti cha hukumu, wakisema mtu huyu huwavuta watu ili wamwabudu Mungu kinyume cha sheria. Na Paulo alipotaka kufunua kinywa chake, Galio akawaambia Wayahudi, kama lingekuwa jambo la dhuluma au la hila mbaya, enyi Wayahudi ingekuwa haki mimi kuchukuliana nanyi; bali ikiwa ni hoja juu ya maneno na majina na sheria yenu, liangalieni ninyi wenyewe, maana mimi sitaki kuwa mwamzi juu ya mambo hayo. Akawafukuza waondoke mbele ya kiti cha hukumu. Nao wote wakamshika Sosthene, mkuu wa sinagogi wakampiga mbele ya kiti cha hukumu. Wala Galio hakuyaona mambo hayo kuwa ni kitu. Baada ya hayo akazidi kukaa huko siku nyingi, kisha akaagana na ndugu akaabiri kwenda Shamu; na Prisila na Akila wakaenda pamoja naye, alipokwisha kunyoa kichwa chake huko Kenkrea; maana alikuwa ana nadhiri."

Paulo alihubiri ubatizo, nz michango yake haipaswi kutolewa nje ya mazingira hayo.

Katika somo hili, ebu tuangalie kwa karibu mazingira tunayopata kauli ya Paulo. Angalia kwamba…

Paulo alikuwa anaongelea tatizo lililokuwa Korinth na tabia zao dhidi ya wahubiri

Waligawanyika.

1 Kor. 1:10-11, "*Basi ndugu nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana ndugu zangu nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, yaa kwamba iko fitina kwenu.*"

Mgawanyiko wao ulikuwa ni matokeo ya "nani kanifundisha".

1 Kor. 1:12, "*Basi maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni wa Paulo, na mimi ni wa Apolo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni wa Kristo.*"

Walikuwa wakidai kwamba, "*Mimi ni wa Paulo*", "*Mimi ni wa Apolo*", nk.

Kama Paulo alivyosema baadae, walikuwa wanafiria sana kwa kiwango cha juu kuhusu waubiri tofauti.

Tabia yao ilikuwa ni ishara ya uchanga. 1 Kor. 3:3-4, "*Kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu? Maana hapo mtu mmoja asemapo, mimi ni wa Paulo; na mwingine , mimi ni wa Apolo, je ninyi si wanadamu?*"

Wahubiri walikuwa ni watumishi wenza. 1 Kor. 3:5-9, "*Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo apandaye si kitu, wala atiaye maji; bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye nay eye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe. Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu; ni jingo la Mungu.*"

Hivyo hawakupaswa kujisifia wanadamu. 1 Kor. 3:21-23, "*Basi mtu ye yote na asijisifie wanadamu. Kwa maana vyote ni vyenu; kwamba ni Paulo, au Apolo, au Kefa; au dunia, au uzima, au mauti; au vile vilivyopo sasa, au vile vitakavyokuwapo; vyote ni vyenu; nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu.*"

Inaonekana kuhusiana na ni nani aliyewabatiza, kama inavyoonekana katika maswali ya Paulo yanayo jirudia. 1 Kor. 1:13, "*Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au je mlibatizwa kwa jina la Paulo?*"

Baadhi kwa uwazi kabisa walidai kwamba waop ni wanafunzi binfsi wa wale waliowabatiza. Hivyo, Paulo alikuwa anashukuru kwamba yeye binafsi alibatiza wachache; shukrani kwamba aliwabatiza watu wa nyumbani mwa Krispo, Gayo, na watu wa nyumbani wa Stefano, mtu asije akadai kwamba alikuwa akibatiza kwa jina lake pekee.

1 Kor. 1:14-15, "*Nashukuru kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu. Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana; zaidi ya hao, sijui kama nalimbatiza mtu yeyote mwingine.*"

Hivyo, Paulo alikuwa anaongelea tatizo lililokuwa Korintho. Je tunapaswa kupotosha ukweli kwamba Paulo hakuubiri ubatizo, au kufikiria kama ni muhimu? Kinyume.

Mahubiri ya Paulo ilisababisha wengi kubatizwa

Luka anaandika kazi ya Paulo Korintho, jinsi alivyo fanya kazi na Akuila na Prisila. Mdo. 18:1-3, "*Baada ya mambo hayo Paulo akatoka Athene akafika Korintho. Akamwona Myahudi mmoja jina lake Akila, mzaliwa wa Ponto; naye amekuja kutoka nchi ya Italia siku za karibu pamoja na Prisila mkewe, kwa sababu Klaudio amewaamuru Wayahudi wote watoke Rumi, naye akafikilia kwao; na kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja, akakaa kwao wakafanya kazi pamoja, kwa maana walikuwa mafundi wa kushona hema.*"

Aliandika jinsi alivyojibizana nao katika Sinagogi, akashuhudiwa kwamba Yesu ni Kristo, na kushinda licha ya kukataliwa na Wayahudi wasioamini. Mdo. 18:4-7, "*Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato, akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani. Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo. Walipopingamana naye na kumkana Mungu, akakung'uta mavazi yake akawaambia, damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi tangu sasa nitakwenda kwa watu wa Mataifa. Akaondoka huko akaingia katika nyumba ya mtu mmoja jina lake Tito Yusto, mcha Mungu ambaye nyumba yake ilikuwa mpaka mmoja na sinagogi.*"

Luka anaandika mafanikio ya mahubiri ya Paulo.

Krispo, kiongozi wa Sinagogi, na nyumba yake waliamini katika Bwana (na Paulo binafsi aliwabatiza).

- Mdo. 18:8, "*Na Krispo mkuu wa sinagogi akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia waliamini, wakabatizwa.*"
- 1 Kor. 1:14, "*Nashukuru kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu ila Krispo na Gayo;*"

Lakini pia "wengi" wa Wakorintho waliamini na wakabatizwa.

Mdo. 18:8, "*Na Krispo mkuu wa sinagogi akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia waliamini, wakabatizwa.*"

Hataivyo Paulo binafsi aliwabatiza wachache, mahubiri yake yalisababisha wengi wabatizwe! Ubatizo lazima ulikuwa na nafasi kubwa katika mahubiri yake. Hiyo ni sababu moja wapo ya kwa nini tusipindishe maneno ya Paulo kwa kanisa la Korintho kama inavyoashiria kuwa haikuwa muhimu. Tunapogeukia katika 1 Kor. 1:13, pia tunapaswa kuangalia kwamba…

Maneno ya Paulo yanaonyesha umuhimu wa ubatizo

Angalia kwa makini kaatika mafundisho ya Paulo. Kwa mtu kujiita mwenyewe kwa Paulo (au mwanadamu mwingine) ilihitajika mambo mawili:

- Paulo angepaswa kusulubiwa kwa ajili ya mtu huyo. 1 Kor. 1:13, "*Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alibatizwa kwa ajili yenu? Au mlibatizwa kwa jina la Paulo?*"
- Mtu angepaswa kubatizwa kwa jina la Paulo.

Hakuna kilichotokea, ndiyo sababu wasingepaswa kujiita wenyewe kwa wanadamu.

Lakini zingatia kile ambacho ubishi wa Paulo unamaanisha chanya…

Kuitwa kwa jina la Kristo, vitu viwili vinahitajika:

- Kristo angepaswa kufa kwa ajili ya mtu huyo (ambayo kimsingi alifanya).
- Mtu ange paswa kubatizwa kwa jina la Kristo!

Je umebatizwa kwa jina la Kristo? Kama siyo, basi huwezi kuitwa kiuhalali kuwa Mkristo!

Katika mazingira haya ya kifungu hiki cha maandiko ambayo wengi wanatumia kudai kwamba ubatizo siyo lazima, Paulo anaeleza kwamba mtu hawezi kuitwa Mkristo wasipobatizwa katika jina la Kristo!

Tunawezaje kuelewa kauli ya Paulo ("*Maana Kristo hakunituma kubatiza, bali kuihubiri injili…*")? Jibu ni rahisi…

Paulo alikuwa anasisitiza wajibu wake kama mtume. Paulo alitumwa kuhubiri, siyo kubatiza.

Kama mtume (ikimanisha "mtu aliyetumwa"), wajibu wa Paulo ilikuwa ni kutangaza injili.

Kama ilivyo tangazwa kwa Waefezo, alipewa jukumu la kuhubiri "*utajiri wake Kristo usiopimika*" Efe. 3:8, "*Mimi niliyemdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahubiri mataifa utajiri wake Kristo usiopimika.*"

Ambayo alifanya kwa uvuvio. Gal. 1:11-12, "*Kwa maana ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya aina ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*"

Hataivyo mahubiri yake yalitokana na ubatizo (Mdo. 18:8), haikuwa halisia kwamba aifanye **yeye** (binafsi).

Wengine wangeweza kufanya ubatizo kirahisi (kama vile wasaidizi wake aliokuwa akisafiri nao); ambayo ilitokeaa Korintho, wakati wengi walikuwa wakibatizwa, yeye binafsi aliwabatiza wachache.

Paulo alitumia mfumo uliozoeleka wa kuongea.

Angalia maneno ya Yesu katika: Yohana 6:27, "*Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa, kwa maana huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba yaani Mungu.*"

Yesu hakusema kwamba mtu hapaswi kufanya kazi, lakini alikuwa anasisitiza umuhimu wa kutafuta mazuri ya kiroho kuliko chakula cha kimwili.

Katika mfumo uo huo Paulo anasema katika 1 Kor. 1:17, "*Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali niihubiri habari njema; wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika.*"

Paulo hakusema kwamba hajabatizwa, bali kwamba wajibu wake kama mtume kuihubiri injili ilikuwa muhimu zaidi!

Jinsi wengine walivyomwelewa Paulo.

- "Kwamba, kutobatiza kama wajibu wangu mkuu. Ubatizo haukuwa mfumo wake wa ajira, hata hivyo alikuwa na wajibu uliozoeleka naa wengine kuwahudumia watu, naa mara nyingi aliifanya." – Maandishi ya Barnes, katika 1 Kor. 1:17).

- "Kulingana na Semitic idiom, 'sio ubatizaji mwingi, kama…'. Neno 'tuma' inavyojumuisha maana 'nifanya kuwa mtume'. Jukumu la msingi la mtume lilikuwa ni 'kutoa ushahidi.'" – Komentari ya Farrar katika 1 Kor. 1:17

- "Ubatizo haukuwa kazi yake maalum, siyo kazi halisi ambayo ilifanya Paulo akatumwa, ilikuwa sehemu ya kazi yake, la sivyo asingewabatiza Krispo, au Gayo, au watu wa nyumbani mwa Stefano, bali kuhubiri ndio ilikuwa kazi yake." – (Poole Annatations, 1 Kor. 1:17).

- "…chukulia akili ya Paulo misemo mingine ya ubatizo, ms. 17 inapaswa kutafsiriwa katika upande wa rasimi wa kuweka hofu katika swala: Kristo alimtuma Paulo kuihubiri Injili kuliko kubatiza. Lakini huu siyo uchakavu wa thamani ya ubatizo." – (Beasley – Murray Ubatizo Katika Agano Jipya, uk. 181).

Hitimisho

Mtu anapozingatia uthibitisho wote tulionao kuhusu hali ya Korintho, tunajifunza…

Wengi walibatizwa kama matokeo ya mahubiri yaa Paulo. Mdo. 18:8, "*Na Krispo mkuu wa sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote. Wakorintho wengi waliposikia waliamini, wakabatizwa.*"

Paulo aalikuwa na furaha kwamba binafsi alibatiza wachache, kwa sababu ya matatizo yaliyoibuka baadae Korintho. 1 Kor. 1:14-15, "*Nashukuru kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu.*"

Katika kifungu watu wengi kwamba ubatizzo siyo muhimu…

Paulo anasisitiza wajibu wake kama mtume. 1 Kor. 1:17, "Nashukuru kwa sababu sikumbatiza mtu kwenu, ila Krispo na Gayo; mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu."

Mawazo ya Paulo unaonyesha umuhimu wa ubatizo (kuitwa kwa jina la Kristo, mtu lazima abatizwe kwa jina la Kristo). 1 Kor. 1:13, "*Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?*"

Kwa nini usiitwe Mkristo kwa uhalali? Kweli, Yesu Kristo alisulubiwa kwa ajili yako; lakini je umebatizwa kwa jina la Kristo?